



**KARAMU
YA
KWANZAA!
KWANZAA CELEBRATION**



**Kwanzaa ni matunda ya kwanza. Sherehe ya siku saba.
Nguzo Saba za Kwanzaa. Kila siku ya Kwanzaa tunawasha mshumaa.
Mshumaa mweusi, mwekundu au kijani.**



**Kwanzaa means first fruits. Seven days of celebration. Seven Principles of Kwanzaa.
We light a candle every day of Kwanzaa. A black, red or green candle.**



Nguzo ya kwanza ya Kwanzaa ni **UMOJA**.



Kwanzaa siku ya kwanza, tunawasha mshumaa mweusi.
Nyeusi ni fahari yetu. Sisi watu weusi. Tuungane pamoja!



The first principle of Kwanzaa is **UNITY**. First day of Kwanzaa, we light a black candle.
Black is our pride. We the Black People. Let's Unite.



Nguzo ya pili ya Kwanzaa ni **KUJICHAGULIA**.



Kwanzaa siku ya pili, tunawasha mshumaa **mwekundu**.

Nyekundu ni mapambano. Tusimamie haki zetu Tuandike historia yetu!



The second principle of Kwanzaa is **SELF-DETERMINATION**. Second day of Kwanzaa, we light a red candle. Red are the struggles. Stand for your rights. Let's write our history.




Nguzo ya tatu ya Kwanzaa ni **UJIMA**.
Kwanzaa Siku ya tatu, tunawasha mshumaa wa **kijani**.
Kijani dunia yetu. Kijani matumaini. Tujenge jamii yetu!



The third principle of Kwanzaa is **COLLECTIVENESS**. On the third day of Kwanzaa we light a green candle. Green is our earth. Green is hope. Let's build our community.



Nguzo ya nne ya Kwanzaa ni **UJAMAA**.
Kwanzaa siku ya nne, tufanye kazi pamoja.
Umoja ni nguvu yetu, utengano ni udhaifu.



The fourth principle of Kwanzaa is **COOPERATION**. Day four of Kwanzaa, let's work together.
Unity is our strength, disunity weakens us.



Nguzo ya tano ya Kwanzaa ni **NIA**.
Kwanzaa siku ya tano, tutunze utamaduni wetu.
Waswahili wanasema, penye nia pana njia!



The fifth principle of Kwanzaa is **PURPOSE**. Day five of Kwanzaa, let's preserve our culture.
The Swahili people say, where there is a will, there's a way!



Nguzo ya sita ya Kwanzaa ni **KUUMBA**.
Kwanzaa siku ya sita, talanta tuzitumie.
Kipaji chako, mtaji wako, kitumie kwa manufaa.



The sixth pillar of Kwanzaa is **CREATIVITY**. Day six of Kwanzaa, let's use our talents.
Your talent, your wealth, use it productively.



Nguzo ya saba na ya mwisho ya Kwanzaa ni **IMANI**
Kwanzaa siku ya saba, amini yote yanawezekana.
Amini kwa moyo wote, unaweza kubadilisha dunia.



The seventh and last principle of Kwanzaa is **FAITH**. Day seven of Kwanzaa, believe all is possible.
Believe with all your heart, you can change the world.

**Furahia Kwanzaa kwa karamu ya siku saba.
Leta mishumaa, mkeka na mazao.
Leta kikombe cha umoja, kinara na zawadi pia.**



**Enjoy Kwanzaa with a seven-day celebration. Bring candles, a mat and harvests
Bring the unity cup, candle holder and gifts too.**

Mwisho tujikumbushe, nguzo saba za Kwanzaa. Umoja, Kujichagulia, Ujima, Ujamaa, Nia, Kuumba na Imani. Mimi na familia, jumuhiya na dunia. Karibu tufurahie, karamu kuu ya Kwanzaa.



Lastly let's recap the seven principles of Kwanzaa. Unity, Self-determination, Collectiveness, Cooperation, Purpose, Creativity and Faith. Me and the family, community and the world. Let's celebrate the great Kwanzaa celebration.

ZOEZI

Chagua jibu sahihi –Pick the right answer

1. Mishumaa ya Kwanzaa ni ya rangi gani?
 - a. Dhahabu, nyeupe na nyeusi
 - b. Nyekundu, nyeusi na kijani
 - c. Njano, kahawia na machungwa

2. Nguzo ya saba ya Kwanzaa ni nini?
 - a. umoja
 - b. imani
 - c. uhuru

3. Nia kwa kiingereza maana yake ni nini?
 - a. Faith
 - b. Freedom
 - c. Purpose



swahili**KIDS**



SwahiliKIDS.COM



[@kiswahiliKIDS](https://www.facebook.com/kiswahiliKIDS)



[@swahiliKIDS](https://www.youtube.com/@swahiliKIDS)



[@swahili.KIDS](https://www.instagram.com/@swahili.KIDS)